



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI 2025

Tunduma, Tarehe 27 Februari 2025.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma, Mariam Chaurembo anapenda kuutaarifu umma kuwa Maadhimisho ya SIKU YA WANAWAKE DUNIANI kimkoa yatafanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe tarehe 08 Machi 2025.

Hivyo, kwa kuzingatia muktadha huo amesema maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 2025 kwa Halmashauri ya Mji Tunduma yatafanyika **Siku ya Jumamosi tarehe 1 Machi 2025** katika Hospitali ya Mji Tunduma iliyopo Mtaa wa Mpemba, Kata ya Mpemba kuanzia saa 02:00 asubuhi. Ambapo mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo, atakuwa Mkuu wa Wilaya ya Momba, Mhe. Elias Mwandobo.

Kiongozi huyo amefafanua kuwa, maadhimisho hayo kwa mwaka huu (2025) yanayoongozwa na Kauli Mbiu isemayo **"Wanawake na Wasichana Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezesaji."**

Hivyo, Wananchi wote mnakaribishwa kushiriki maadhimisho hayo ambayo yataambatana na shughuli za kijamii zitakazofanywa na Wajasiriamali, Wadau wa Maendeleo pamoja na Makundi mbalimbali ya Wanawake katika jamii.

Benton J. Nollo

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Mji Tunduma

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji, Tunduma S.L.P 73 Simu Na: 025 295 7388, Nukushi:025 295 7391, Barua
Pepe:td@tundumatc.go.tz, Tovuti:www.tundumatc.go.tz